1013/1
P1 KISWAHILI
Karatasi ya 1
MACHI/APRILI 2019
MUDA: SAA 2

# MTIHANI WA MWIGO 2019
# KISWAHILI KARATASI YA 1
# SAA 2

*Maagizo*

*Karatasi hii ina sehemu NNE: Insha, Ufahamu, Matumizi ya Lugha na Sajili. Jibu maswali yote katika nafasi ulizoachiwa ndani ya karatasi hii*

*Andika jina, nambari na darasa katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

Kwa matumizi ya mtahini pekee

| Sehemu | Swali | Alama | Upeo |
|---|---|---|---|
| A | 1 | 20 | |
| B | 2 | 20 | |
| C | 3 | 30 | |
| | 4 | 20 | |
| D | 5 | 10 | |
| Jumla | | 100 | |

*Karatasi hii ina kurasa 11 hakikisha karatasi zote zimepigwa chapa.*

## A ) SEHEMU YA KWANZA: INSHA (AL. 20)

1. Andika insha isiyopungua maneno 300 kuhusu moja wapo ya mada hizi .
   a) Ulihudhuria mkutano ulioitishwa na Bwana Chifu kuhusu mikakati ya kudhibiti mimba za mapema miongoni mwa vijana. Andika kumbukumbu za mkutano huo.
   b) Andika kisa kinachoafiki methali hii :mwana akibebwa hutazama kisogo cha ninake.
   c) Umealikwa katika sherehe ya kuadhimisha siku ya mazingira duniani kama mgeni wa heshima. Andika hotuba utakayotoa kuhusu uharibifu wa mazingira na madhara yake katika jamii.
   d) Andika insha itakayokamilika kwa maneno haya..........nilipolala pale kitandani jioni ile machozi ya furaha yakinitiririka sikuwa na budi ila kumshukuru Rabana kwa siha njema.

**SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (ALAMA 20)**

**2. *Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali*.**

Binadamu wana mazoea ya kufikiria kuwa jinsi wafanyavyo , waongeavyo na wafikiriavyo kuhusu vitu ndivyo inavyopasa kuwa. Kama binadamu tunaamini njia yetu ndiyo sahihi, yenye mantiki na inayopaswa kufuatwa na kila mtu. Msingi huu huu unakwenda kinyume na kutambua kila binadamu ana haki ya kusema, kufikiri au kuongea na kutenda mradi asikiuke haki ya mwenzake iliyo sawa na yake. Nguzo mojawapo *inayogongomelea* hoja hii ni Haki za Binadamu.

Azimio la kutangaza Haki Bia za Binadamu liliafikiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 10 Desemba, 1948. Baraza Kuu hilo liliyasisitizia mataifa wanachama umuhimu wa kuyasambaza, kueneza na kusisitiza kusambazwa kwa Azimio hilo katika shule na taasisi za kielimu. Msingi wa uhuru, haki na amani ulimwenguni ni kutambua binadamu wote wana haki sawa. Ingawa kimsingi jamii na mataifa yote ya ulimwengu yanapaswa kutathmini, kusambaza na kuhimiza umuhimu wa Haki za Binadamu zipo jamii ambazo hukiuka haki hizo. Matokeo ya ukiukaji huu yana athari hasi sana kama ilivyotokea nchini Rwanda na Bosnia Herzegovina kulikotokea mauji ya halaiki.

Azimio la Haki za Binadamu linajumuisha vipengele kadha ambavyo ni mihimili mikuu ya azimio lenyewe. Kipengee msingi kabisa kinasisitiza kuwa kila kiumbe anazaliwa huru na ana haki na hadhi sawa na kiumbe mwingine.Ukweli wa kauli hii ulikokotezwa na kauli ya mwanafalsafa maarufu Jean Jacques Rosseau aliyesema kuwa kila kiumbe huzaliwa huru lakini huwa katika pingu ulimwengu mzima. Kauli hii ilitambua ukiukaji huu wa kipengele hiki. Kipengele cha pili kinasisitiza kuwa binadamu wote wana haki za kufurahia uhuru wao pasi na kutengwa au kubeuzwa kwa misingi yoyote ile si rangi, kabila, jinsia, lugha, dini, asilia, utajiri, au chochote kile.

Vipengele vingine vinatukumbusha kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na kupata ulinzi. Hamna mtu anayepaswa kuishi maisha ya utumwa au unyonge wa kutumikishwa kwa namna yoyote ile. Suala hili linasisitizwa na kipengele cha sita kinachokataza kudhalilishwa kwa watu au kutunzwa kwa namna yoyote ambayo inamfedhehesha kama kiumbe. Azimio la Haki za Binadamu linasisitiza kuwa binadamu yoyote yule ana haki ya kupata ulinzi wa kisheria.. Binadamu huyo hapasi kubaguliwa na ana haki ya kupata fidia ya kisheria taraa haki zake za kimsingi zikikiukwa.

Hata hivyo sio watu wote ulimwenguni amabao wanazifurahia haki hizi za kimsingi. Zipo *lukuki za jamii* ulimwenguni ambako haki za kimsingi zinakiukwa. Katika nchi ambazo zinaongozwa na watawala wa kiimla, si ajabu kuona haki za bianadamu zikikiukwa. Viongozi wa aina hiyo huwa wamegeuzwa ng’ombe wa shemere na tamaa,ubinafsi na ukatili usiojua thamani ya utu.

Viongozi wa aina hii wanasahau kuwa kila binadamu ana haki ya kuishi maisha huru, asipotumikishwa wala kulanguliwa kama bidhaa.

Nchi za kiimla aghalabu huongozwa na itikadi kuwa kiongozi ndiye pekee ambaye ana uwezo wa kufikiri, kuamua na kutenda. Watu wengine wanapaswa kumfuata kisilka kama yule mbwa wa Pavlov ambaye alitokwa na mate kila kengele ilipopigwa. Viongozi wa aina hii hawachelei *kuwatenza nguvu* raia zao; kuwadhalilisha kwa namna nyingi. Viongozi wa aina hiyo huiona sheria ya nchi kama iliyowekwa kwa watu wengine bali sio wao. Msimamo huu unakwenda kinyume na kipengele cha saba cha Haki Bia za Binadamu kisemacho kuwa wote ni sawa mbele ya sheria.

Baadhi ya haki zinazokiukwa katika jamii za kimabavu ni haki ya watu kuungana, kuwaza, kushiriki katika maamuzi ya serikali, kuwa mwanachama wa jumuia aitakayo,kumiliki mali, kutembea, kuishi anakotaka, kutohukumiwa bila ya kuwako na utaratibu wa kisheria. Ni muhimu hata hivyo kujua ni muhimu kwa raia wenyewe kujielimisha na kuzijua haki zao. Serikali inapaswa kuwa mlinzi wa sheria zenyewe. Lakini muhimu kujua pia kuwa mlinzi naye hulindwa pia.

<u>Maswali</u>

a) Ipe makala hii anwani mwafaka (al.2).

b) Onyesha namna maoni ya binadamu yanavyoenda kinyume na haki za binadamu (al.3)

c) Kulingana na Haki Bia za Binadamu, taja msingi wa uhuru na haki duniani (al.2)

d) Eleze vipengele vitatu vinavyohimili Azimio la Haki za Binadamu (al.6).

e) i) Taja mambo manne katika taarifa yanayoonyesha ukiukaji wa Haki za binadamu(al.4)

ii) Andika athari moja ya ukiukaji wa Haki za Binadamu kulingana na taarifa (al.1).

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katka taarifa (al.2)

inayogongomelea hoja ____________________________________________________________

lukuki za jamii ____________________________________________

## C. MATUMIZI YA LUGHA(al. 50)

### 3. SARUFI

a) Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya A-WA (al.2).

b) Andika tofauti moja kati ya sauti hizi (al.2)

i) /v/ na /f/ ______________________________________________________________

ii) /m/ na /n/ ______________________________________________________________

c) Andika sentensi hii upya kwa kugeuza maneno yaliyopigwa mstari kuwa nomino (al.2).

Mhalifu **<u>alisamehewa</u>** kwa sababu ya **<u>kunyenyekea.</u>**

d) Tumia kihusishi **juu ya** katika sentensi kama kielezi (al.1).
e) Andika sentensi hii kwa wingi (al.2)
Seremala alilainisha ubao huo akitengeneza meza.
f) Tumia kiambishi **a** cha wakati katika sentensi (al.2).
g) Onyesha aina za maneno katika sentensi hii (al.2).
Mwanafunzi mkakamavu huzingatia masomo sana.

h) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi hii (al.2).
Mhunzi alimfulia mjukuu wake pete ya shaba.
i) Andika sentensi hii upya katika hali ya ukanushaji kwa kutumia nge au ngali (al.2).
Mwajiri aliwatesa wafanyikazi. Alishtakiwa kwa unyanyasajiwa waajiri.
j) Andika sentensi hii kwa msemo wa taarifa (al.2)
"Kusoma kwa mapana kutapalilia ubunifu wa wanafunzi hawa wenu", mtaalamu akatwambia.
k) Akifisha sentensi hii (al.4).
mbona hamjakamilisha kazi yangu mwalimu aliwauliza wanafunzi tulitumwa nyumbani ndio maana hatukukamalisha akajibu kiranja
l) Sahihisha sentensi hii (al.1)
Mwenye amechukua kitabu yangu anipee
m) Changanua sentensi hii kwa kutumia mshale (al.3).
Rehema alinitembelea jana jioni lakini sikuwepo.

n) Kaumu amewafanya ng'ombe wangu wanywe maji. Andika sentensi upya bila kutumia 'amewafanya' (al.1)
o) Andika nahau inayoelezwa na maneno haya (al.2)
oa ___________________________
omba ______________________________

**4. Msamiati**

a) Sehemu mahakamani asimamapo mshtaki, mshatikwa au shahidi ________________ (al.1).
b) Mtu atunzaye wanyama wanaopandwa kama vile farasi au punda ________________ (al.1).
c) Utamwitaje mtoto wa ndugu yako? ___________________ (al. 1).
d) Tumia majina ya makundi kukamilisha sentensi hii.
Akina mama hao walitunukiwa ________ ya leso. (al.1).
e) Tunga sentensi moja kubainisha matumizi ya **rithi** na **ridhi** (al.2).
f) Andika methali inayoafiki maelezo haya (al.2).
Ukiona mambo yanaenda vizuri jua kuna mtu ameshughulika sana ili mambo yatengenee.
g) Ala ya muziki mfano wa sanduku hutengenezwa kwa mbao na vibao vyembamba hutandikwa ________________________________ (al.1).
h) Ni mnyama mdogo kama kima lakini mwenye rangi ya kijivu, huharibu sana mimea shambani ____________________ (al.1).
i) Ng'ombe ni kwa kwato, binadamu wayo, na simba ni kwa ________________ (al.1).

j) Sehemu ya shule inayotumiwa kufanyia michezo ______________________ (al.1).
k) Utandabui mweusi utokanao na moshi jikoni huitwa ___________________ (al.1).
l) Nguo inayotumiwa kusetiri uchi wa maziwa ya mama ___________________ (al.1).
m) Machwa ni wakati gani ? _______________________________________ (al.1).
n) Andika tarakimu hii kwa maneno 1,679,893 (al.1).
o) Malipo anayolipa mpangajii kama kodi ya nyumba ________________________ (al.1).
p) Kikundi cha wasafiri _______________________ (al.1).
r) Mchezo wa watoto wa kujificha na kutafutana huitwaje? _____________________ (al.1).
s) Kikembe cha simba huitwaje? __________________________ (al.1).

**5. Sajili**
a) Eleza sifa nne za lugha ya wazee (al.4)

b) Taja vigezo vitatu vinavyotumiwa kuteua lugha rasmi (al.3).

c) Ni kwa nini waafrika walipinga usanifishaji wa Kiswahili wakati wa ukoloni (al.3)